

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"  
Telephone: + 028 2750271  
Fax: + 028 2750376  
E-mail: [ded@maswadc.go.tz](mailto:ded@maswadc.go.tz)



S.L.P 170,  
MASWA,  
SIMIYU.

Kumb.Na. MDC/ADM/10/30/VOL 1/86

25 Machi, 2022

**YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kupitia kibali cha ajira mbadala Kumb. Na.FA.170/533/01"B"/71 cha tarehe 10 Februari 2022, kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatangaza nafasi wazi Sita [6] za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III.

**1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 6**

**1.1. Sifa za Mwombaji:-**

- Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha [NTA Level 5] au Certificate katika moja ya fani zifuatazo.
- Utawala
- Usimamizi wa Rasilimali watu
- Maendeleo ya Jamii au
- Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- (iii) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (iv) Awe na cheti cha kuzaliwa.

**1.2. MAJUKUMU YA KAZI**

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji.
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raha na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- (v) Kutafasiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- (viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- (ix) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.

- (x) Kupokea, kusikiliza na kutafua malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
- (xi) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- (xii) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- (xiii) Kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri.

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA

**Mshahara:** Ngazi ya TGS B kwa mwezi.

### 3.0. MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji waambatanishe na nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

### 4.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,  
S.L.P. 170,  
**MASWA –SIMIYU.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **07.04.2022 Saa 9.30 Alasiri.**

**NB:**

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.maswadc.go.tz](http://www.maswadc.go.tz) Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz) na katika mbao za matangazo za Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.



Vivian M. Christian  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
MASWA**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA